JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA KATIKA SHULE ZA MSINGI KWA KADA YA ELIMU CHINI YA MRADI WA GPE - TSP**

Mradi wa Kuboresha Kada ya Ualimu (*Global Partnership for Education Teacher Support Programme – GPE - TSP)* kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) inatekeleza afua mbalimbali ikiwemo ya kuratibu upatikanaji wa Walimu wa Kujitolea (engagement of volunteer teachers). Mradi huu unatangaza nafasi za kujitolea kwa walimu **694** wa Shule za Msingi watakaofanya kazi chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika shule zenye uhitaji mkubwa zaidi kwa kuzingatia utaratibu wa kupanga walimu wa Shule za Msingi '*Primary Teacher Allocation protocol (P – TAP)*´ambao umeanishwa kwenye Andiko la Mradi huo wa GPE – TSP.

Hivyo, wahitimu kutoka Vyuo vya Ualimu na vinavyotambuliwa na Serikali wanatangaziwa kutuma maombi ya kujitolea katika Shule za Msingi mbalimbali kama zilivyoanishwa katika Mfumo wa *'Online Teachers Application System (OTEAS)'* kuanzia tarehe **17 Mei - 30 Mei, 2025.** Nafasi zilizopo ni kwa wahitimu wa Astashahada (Certificate) na Stashahada (Diploma).

## 1.0 TARATIBU ZA KUOMBA

Walimu wote wenye sifa watume maombi kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha ***ajira.tamisemi.go.tz***. Tangazo hili linawahusu wahitimu wa Kozi za Ualimu kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2023.

## 2.0 SIFA ZA KITAALUMA ZA MWOMBAJI

Walimu wanaoomba kujitolea katika Shule za Msingi wanatakiwa kuwa na sifa za kitaaluma kama ifuatavyo:

(i) **Mwalimu Daraja la III A** - Mwenye Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi (Certificate in Primary Education);
(ii) **Mwalimu Daraja la III B** - Mwenye Stashahada (Diploma) ya Ualimu aliyesomea Elimu ya Awali; na
(iii) **Mwalimu Daraja la III B -** Mwenye Stashahada (Diploma) ya Ualimu aliyesomea Elimu ya Msingi.

## 3.0 MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI WA KAZI

(i) Awe raia wa Tanzania;
(ii) Awe na umri usiozidi miaka 43;
(iii) Aambatishe nakala ya cheti cha: Kuzaliwa, Kidato cha nne au sita, na Mafunzo ya Fani ya Ualimu.
(iv) Awe tayari kufanya kazi katika Shule za Msingi zenye mahitaji makubwa zaidi ya walimu wa kujitolea zilizopo pembezoni;
(v) Asiwe Mwajiriwa wa Serikali au Taasisi nyingine;
(vi) Awe hajawahi kufukuzwa au kustaafishwa katika Utumishi wa Umma kwa makosa ya kiutumishi;
(vii) Awe na Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA);
(viii) Waombaji waambatishe nyaraka zote muhimu katika mfumo; na (ix) Waombaji wote waliosoma Elimu ya Sekondari nje ya nchi wanatakiwa kupata Namba ya Ulinganifu wa Matokeo (Equivalent Number) inayoanza na Herufi **EQ…** kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

Kwa maelezo ya ziada kuhusiana na sifa za waombaji na taratibu za utumaji wa maombi tafadhali kupitia: ***www.tamisemi.go.tz*** au wasiliana na kituo cha huduma kwa wateja cha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa namba za simu *026 2160210 au 0735 160210.* Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **30 Mei, 2025 saa 05:59 usiku.**

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ifuatayo**:** ***www.tamisemi.go.tz.***

**Limetolewa na:**

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 1923,
**41185 DODOMA.**

**17 Mei, 2025**